

**Dondoo za mkutano wa pili wa Umma wa WApanda Baiskeli Dar es Salaam  
Tarehe 4 februari 2006**

**Waliohudhuria**

Abdallah Khatib

Elaine Baker

Paulo Atibu

John Emil Maximilian

Juma Ali Salehe Jongo

Shukuru Hassan

Siyenu Mohammed

Tendekayi Guni

**Wajibu wa utawala ulijadiliwa**

- Ilikubalika kuwa usajili upewe nafasi ya kwanza
- Ilikubalika kufungua akaunti benki.
- Wajumbe walihamasishwa kutoa mchango wa hiari kwa matumizi ya utawala na usajili. Ilikubalika kuwa na kitabu cha risiti kwa michango hiyo.
- Ilikubalika kukutana tena wiki iliyofuata saa 3 asubuhi, lakini kwa wiki zitakazofuata mkutano ufanyike saa 9.30 alisiri kila jumamosi ili kuwasaidia wale wanaofanya kazi jumamosi asubuhi.

**Ufuatiliaji**

- Elaine na Meja kuamua ofisi ilipo na ufuatiliaji wa barua za usajili kutoka kwa katibu kata.
- Maximilian kwenda kwenye ofisi ya Makamu wa rais kufuatilia kuhusu usajili wa NGOs
- Meja, Elaine na Maximilian kutoa nakala za CVs na picha za pasipoti kwa ajili ya usajili .
- Elaine kuchapa vipeperushi kwa muda wa wiki mbili ili wapewe kwa wajumbe wavigawanye kwa wengine.

**Tulizungumzia kazi zitakazofanywa na UWABA. Yifuatazo ni mawazo yaliyojadiliwa:**

- Kujadili kama kikundi ili kupata bima kwa wapanda baiskeli
- Kutoa matangazo kwenye magazeti na kufanya mkutano na vyombo vya habari kuhusu UWABA.
- Kubuni nembo.
- Kuchapa t-shirts ili wajumbe wanunue. Shukuru Hassan alisema itawezekana kuzipata kwa sh 2,200 kila moja.
- Kutafuta watoto watakoingia kwenye mashindano ya insha ya baiskeli (maelezo yalizungushwa )
- Kutafuta wataalam kutoka chuo kikuu ili kuzungumzia haki za wapanda baiskeli /au mpango jiji kwa wapanda baiskeli.
- Kuwahamasisha wanafunzi wa sheria na uhandisi/mipango ndani ya Tanzania na nje kufanya utafiti kuhusu hali ya wapanda baiskeli Dar es Salaam.

- Kuanzisha vyeti vya "maeneo rafiki ya wapanda baiskeli " na vigezo vitakavyomwezesha afisa kuomba.

Ufuatiliaji:

- Maximilian afuatilie kuhusu mkutano na vyombo vya habari
- Tendekayi kubuni nembo
- Elaine kuandika matangazo